BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE HABARI NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE , WANAWAKE NA WATOTO - 2020/2021**

---

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu , ambae ametuwezesha sisi kukutana hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa katika hali ya uzima na afya njema. Lakini pia, ningependa kwa heshima na taadhima, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya chombo hiki muhimu cha wananchi kueleza maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee , Wanawake na Watoto kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, kazi hii ya kupitia bajeti ambayo inalenga kuleta maendeleo katika nchi yetu, isingewezekana kama tusingepata mashirikiano yako ya dhati, pamoja na Wajumbe wangu wa Kamati wakisaidiwa na Sekretariati ya Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ambao kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifutavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | M/Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Makame Said Juma | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Omar Seif Abeid | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| *9.* | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| *10.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Msaidizi |
| *11.* | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi , ilipata fursa ya kulifikiria kwa kulifanyia uchambuzi wa kina fungu la makadirio ya bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto ikiwa ni kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 96 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hiyo nachukuwa nafasi hii kukuarifu kuwa kazi hiyo tuliifanya kwa umakini wa hali ya juu na leo hii tupo hapa kukuwasilishia kazi tuliyoifanya kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 96 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016 kwamba:-

**Mheshimiwa Spika** , kuanzia na ufafanuzi wa tathmini ya jumla iliyofanywa na Kamati yangu kuwa makadirio ya Makusanyo ya Wizara hii yamezidi kutoka shilingi **1,039,464,000** kwa mwaka wa fedha unaomalizika hadi kufikia shilingi **2,108,555,000** kwa mwaka ujao wa fedha wa 2020/2021. Hii ni dalili kwamba Wizara imejipanga kuiongezea zaidi mapato Serikali, hatua ambayo Kamati yangu inaipongeza. Hata hivyo, Kamati yetu inaishauri wizara kuongeza bidii zaidi ya utendaji ili kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato yaweze kufikiwa kwani hadi tunapitia bajeti hii wizara imeripoti kufanikiwa kwa asilimia **58%** ya makusanyo kwa mwaka huu wa fedha unaomalizika.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imeonekana kuongeza makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na kazi za Maendeleo , ingawa si kwa asilimia kubwa sana, ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikuwa ni shilingi **17,299,600, 000** ukilinganisha na makadirio ya mwaka wa fedha

2020/2021 ambayo ni shilingi **18,510,451,000** . Mheshimiwa Spika, ni imani ya Kamati kwamba ongezeko hili la fedha limelenga kuleta ufanisi katika kazi kwa Wizara hii na serikali yote kwa jumla.

## PROGRAMU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**Mheshimiwa Spika** , Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa Wizara kwa kusimamia vyema utekelezaji wa programu ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, kwani sote tumekuwa tukishuhudia uimarishwaji wa mipango ya upatikanaji wa mikopo nafuu ikiwa na lengo la kuimarisha kwa kuwajengea uwezo wajasiriamali wetu. Aidha , Kamati inaridhika na juhudi za wizara za kuimarisha na kukuza hadhi za kiuchumi kwa wazee, vijana, wanawake watoto na makundi mengine katika jamiii, suala ambalo limepelekea matokeo mazuri ya viashiria vilivyowekwa katika utekelezaji wa programu hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inaitakia Wizara kila la kheri na kufanikisha mipango iliyojiwekea katika mwaka ujao wa fedha ikiwa ni pamoja na kukusudia kutoa mikopo 700 yenye thamani ya shilingi Milioni Mia Nane na Hamsini El (**850,000,000**) kwa lengo lile lile la kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu pia inachukuwa nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kusimamia mradi kwa vijiji vilivyounganishwa kwa umeme wa jua ambapo tathmini ya mradi huo imebaini kwamba, Mradi huo umewasaidia wananchi kung'arisha vijiji vyao na kuweza kuwasaidia katika kuwawezesha watoto kudurusu masomo yao wakati wa usiku na kujiongezea kipato kwa '***Solar Mama'.*** Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara katika malengo yake ya mwaka ujao wa fedha, kuongeza idadi ya kinamama watakaowapatia mafunzo ya utengenezaji wa vifaa vya umeme wa jua pamoja na idadi ya watakaowezeshwa kujikwamua kimaisha kupitia kituo cha **Barefoo**t Kinyasini Kibokwa, kutokana na umuhimu wa viashiria hivyo na mafanikio yanayopatikana hasa vijijini.

## PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII NA MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO.

**Mhesimiwa Spika**, Kamati pia imeguswa na kilio cha Wizara hii na jamii kwa ujumla, kwa kukerwa na kuchukizwa sana na vitendo vya baadhi ya akinamama kwa kuwatupa watoto wao baada ya kujifungua. Tunaendelea kuungana na Wizara kutoa wito kwa jamii kuendeleza zaidi mshikamano wa kijamii pamoja na kuendeleza mshikamano wa kifamilia na kuwasaidia

kwa kila hali na kuwa karibu na wanawake wanapokuwa wajawazito, ili kuepusha msongo wa mawazo unaopelekea kufanyika kwa vitendo vya ukatili kwa watoto.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu pia imepata faraja kutokana na azma ya Wizara ya kufuatilia uwezekano wa kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi hapa Zanzibar. Kamati inaamini kwamba, uanzishaji wa mfumo huo unaweza ukawa ni suluhisho la malipo ya Fidia kwa wafanyakazi watakaoumia au kuuguwa wakiwa kazini. Mheshimiwa Spika, Kamati yetu iliwahi kutembelea Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi wa Tanzania Bara na kubaini kwamba, umekuwa ukiwasaidia sana wafanyakazi kwa kugharamiwa matibabu kwa wanaoumia au kupata maradhi wakiwa kazini pamoja na malipo kwa msaidizi wa mgonjwa.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeainisha viashiria kadhaa vinavyolenga matokeo mazuri ya Huduma za kuratibu masuala ya Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake, ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwapatia wanawake mafunzo ya kuelewa haki zao, pamoja na kuwahamasisha kugombea nafasi mbali mbali za uongozi na ngazi za maamuzi. Hili ni jambo zuri ukizingatia ya kwamba, hivi sasa tupo katika vuguvugu la kuelekea

Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba mwaka huu ambapo tutakuwa na chaguzi mbali mbali ikiwemo Uwakilishi, Ubunge na Madiwani. Hapa tunachukuwa fursa hii kuiomba sana wizara kuifanya shughuli hii haraka mara tu watakavyoingiziwa fedha, ili kuimarisha maendeleo ya wanawake na kukuza muitikio wa kuelewa haki za mwanamke, ushirikishwaji na uongozi. Tunawaomba waheshimiwa wajumbe sote tukubaliane na maombi ya Wizara kwa kuidhinisha jumla ya shilingi **1,009,759,061** kwa ajili ya Programu ya Maendeleo ya Wanawake na Kupinga Udhailishaji.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI UKAGUZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Maendeleo ya Wanawake , Habari na Utalii imeshangazwa na uamuzi wa Wizara wa kushusha makadirio ya matumizi kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote kutoka shilingi **1,688,300,000** kwa mwaka wa fedha unaomalizika hadi shilingi **1,484,900,000** kwa mwaka ujao. Kamati inadhani kuipunguzia fedha programu hii wakati huo huo ikizidishiwa kazi ya kukusanya zaidi ni kuibebesha mzigo mkubwa Kamisheni ya Kazi. Tunaishauri Wizara iangalie tena mgawanyo wa fedha kwa taasisi zake ukizingatia ya kwamba Wizara

inategemea sana vianzio vya mapato vilivyochini ya Kamisheni ya kazi kwa ajili ya mapato yake.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda nichukuwe fursa hii , kuipongeza Wizara , akiwemo Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote wa ngazi za juu, pamoja na wa ngazi ya chini, kwa mashirikiano yao waliyotupa katika Muda wa wote wa kazi za Kamati . Ni imani yangu kwamba mashirikiano haya yataimarishwa, ili kuleta ufanisi na kuweza kufikia lengo la kuleta maendeleo katika jamii na Taifa kwa ujumla.

Nawashukuru sana wajumbe wa Kamati yangu kwa kuniamini na mashirikiano makubwa waliyonipa wakati wote nilipokuwa naongoza Kamati hii. Namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie mafanikio mema Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili kutimiza malengo yao waliyokusudia na pia nawatakia kila la kheri wale wote tutakaojaaliwa kuendelea kukitumikia chombo hiki muhimu cha wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa nakushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu nitumie muda wako adhimu ili kuwasilisha hotuba hii. Naamini haya yote yanafanyika ili kuisaidia serikali kufikia malengo iliyojiwekea ya kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

**Mheshiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

**Ahsante.**

**...................................**

**(Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis)**
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii,**
**Baraza la Wawakilishi**.
**Zanzibar.**